



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 02 Juni, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

147. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Miongoni mwa athari zilizosababishwa na mabadiliko ya tabianchi ni kukauka kwa baadhi ya mito, hali inayoleta athari mbali mbali katika ustawi wa maisha ya mwanaadamu.

Je, ni mito mingapi imekauka kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kwa kiasi gani inaathiri jamii zinazoizunguka mito hiyo.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

97. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na malalamiko yanayoendelea kuhusiana na utaratibu na upatikanaji wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi (ZanID) ukilinganisha na utaratibu unaoeleweka wa upatikanaji wa Vitambulisho vya NIDA, huku Serikali ikitoa kauli kwamba kuna vitambulisho vilivyo tayari bila ya kuchukuliwa ilhali wananchi wengi wakifuata vitambulisho vyao wanaarifiwa

kutokuwepo tayari kwa vitambulisho hivyo. Aidha, hivi karibuni Serikali imetoa kauli kwamba kuna wananchi wengi wenye vitambulisho vya ZanID visivyo stahiki yao.

- (a) Je, ni vitambulisho vingapi hadi sasa Kiwilaya ambavyo viro tayari na havijachukuliwa na wahusika.
- (b) Je, Serikali inatumia utaratibu gani bora kuhakikisha kwamba mara tu kitambulisho kinapokuwa tayari mwananchi anaarifiwa na taarifa zinakuwa za uhakika.
- (c) Je, Serikali haioni haja ya kuyachapisha Kiwilaya majina yote ya wananchi ambao vitambulisho vyao viko tayari ili kuwahimiza kuvichukua.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

219. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa kazi kubwa ya kuzifanya ukarabati skuli kongwe za Haile Sellasie na Ben Bella. Lakini ndani ya jimbo la Kikwajuni ipo skuli nyengine kongwe ya Kiswandui ambayo nayo inahitaji kufanyiwa ukarabati au kujengwa jengo jipya la ghorofa.

- (a) Je, Serikali inao mpango wa kuijenga skuli ya Kiswandui kuwa ya ghorofa ili kuleta mandhari na haiba nzuri katika eneo hilo.
- (b) Kwa kuwa eneo la Kiswandui limekuwa na majengo ya ghorofa yanayovutia ikiwemo Ofisi Kuu ya CCM Zanzibar, Je, Wizara haioni umuhimu na ulazima wa kuifanya skuli ya Kiswandui ya ghorofa ili kuongeza nafasi kwa wanafunzi na mazingira mazuri ya kufundishia.
- (c) Je, Serikali ipo tayari kuingiza mpango wa ujenzi wa skuli ya Kiswandui kuwa ya ghorofa katika bajeti ijayo.

Wizara ya Afya:

209. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kama zilivyo Serikali za nchi nyingi duniani, Serikali yetu pia imekuwa ikijipanga kupiga vita na kujiweka tayari dhidi ya maradhi ya mripuko. Hata hivyo, maeneo, fedha, vitengo na miongozo iliyopo haitoshelezi kupiga vita maradhi hayo.

- (a) Je, ni upi mpango wa Serikali wa muda mrefu wa kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuweka na kuhudumia waathirika wa maradhi ya miripuko.

- (b) Je, ni ipi hali ya Mfuko Maalumu wa Dharura kwa ajili ya maradhi ya miripuko.
- (c) Je, ni upi muongozo wa karibuni wa kushughulikia na kuangamiza visababishi vyta maradhi ya mripuko yanayojirejea rejea kama kipindupindu.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

58. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa muda mrefu sana wananchi wa vijiji vyta Gombe, Patini na Nguuni wamekosa huduma ya umeme pamoja na kupeleka maombi yao kwa muda mrefu na mara nyingi sana.

Je, Wizara yako inawaambia nini wananchi hawa.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Afya:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
02 Juni, 2023.



(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA